# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI

## KIKAO CHA KWANZA

**31 JANUARI, 2023**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

_______________

## MKUTANO WA KUMI

## KIKAO CHA KWANZA – TAREHE 31 JANUARI, 2023

**I. WIMBO WA TAIFA NA WIMBO WA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI:**

**II. DUA KUSOMWA NA KIKAO KUANZA SAA 3:00 ASUBUHI:**

**III. KIAPO CHA UAMINIFU:**

Mhe. Abdul Yussuf Maalim

**IV. TAARIFA YA SPIKA:**

**V. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2022.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2022.

## VI. MASWALI:

**OFISI YA WAZIRI MKUU:**

1. **MHESHIMIWA DKT. THEA MEDARD NTARA (VITI MAALUM):**

   Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

   Je, ni lini Serikali itatangaza kima cha chini cha mishahara kwa Wafanyakazi wa Serikali na mashirika binafsi.

**OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

2. **MHESHIMIWA MARIAM NASSOR KISANGI (VITI MAALUM):**

   Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

   Je, kuna mpango gani wa kuongeza na kujenga maeneo ya kusubiri kuona Wagonjwa katika Hospitali nchini.



PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA

3. **MHESHIMIWA LEAH JEREMIAH KOMANYA (MEATU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itapandisha hadhi Shule ya Sekondari ya Nghoboko kuwa ya Kidato cha Tano na Sita.

4. **MHESHIMIWA NDAISABA GEORGE RUHORO (NGARA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itapeleka fedha kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa Hospitali ya Wilaya Ngara.

## OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):

5. **MHESHIMIWA RAMADHAN SULEIMAN RAMADHANI (CHAKECHAKE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):-

Je, kuna mpango gani wa kuhakikisha Shehia zote 388 Zanzibar zinanufaika na mpango wa TASAF kwa 100% badala ya 70%.

**WIZARA YA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:**

**6. MHESHIMIWA FESTO RICHARD SANGA (MAKETE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara:-

Je, nini mkakati wa Serikali kuondoa changamoto ya lumbesa kwa Wakulima wa zao la Viazi nchini.

**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:**

**7. MHESHIMIWA BUPE NELSON MWAKANG'ATA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, ni lini Serikali itajenga josho katika Kata ya Miula Wilayani Nkasi.

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

**8. MHESHIMIWA FLATEI GREGORY MASSAY (MBULU VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, kuna mkakati gani wa kudhibiti matukio ya ubakaji wa Akina Mama uliokithiri katika Jimbo la Mbulu Vijijini.

9. **MHESHIMIWA OMAR ISSA KOMBO (WINGWI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, ni lini Serikali itajenga Ofisi ya NIDA katika Wilaya ya Micheweni.

**WIZARA YA KILIMO:**

10. **MHESHIMIWA SAASHISHA ELINIKYO MAFUWE (HAI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kudhibiti Madalali wanaodalalia mazao ya Wananchi yakiwa shambani kwa bei wanazozitaka.

**WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:**

11. **MHESHIMIWA BENAYA LIUKA KAPINGA (MBINGA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, ni lini Kata za Kiangamanka, Ukata, Kipololo na Kijiji cha Kiwongo zitapelekewa Mawasiliano ya Simu.

## WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:

**12. MHESHIMIWA AMOUR KHAMIS MBAROUK (TUMBE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni kwa nini mizigo ya Wasafiri kutoka Dar es Salaam kwenda Zanzibar kwa kutumia meli kubwa inapekuliwa na Mbwa badala ya *scanner.*

## WIZARA YA MAJI:

**13. MHESHIMIWA DANIEL BARAN SILLO (BABATI VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza mradi wa maji wa Darakuta hadi Minjingu.

**14. MHESHIMIWA JULIANA DANIEL SHONZA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, hadi sasa mpango wa kutatua kero ya Maji katika Mji wa Tunduma umefikia hatua gani.

**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

**15. MHESHIMIWA MAIMUNA AHMAD PATHAN (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:-

Je, ni lini Serikali itamaliza migogoro ya Wafugaji na Wakulima katika Wilaya za Liwale, Nachingwea na Kilwa.

**WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:**

**16. MHESHIMIWA CONDESTER MICHAEL SICHALWE (MOMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki:-

Je, Serikali haioni kuna haja ya nchi yetu kurudi COMESA.

**WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:**

**17. MHESHIMIWA HUSNA JUMA SEKIBOKO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo:-

Je, ni upi mkakati wa Serikali katika kuziendeleza Timu za Michezo za Watoto.

**WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:**

**18. MHESHIMIWA HALIMA JAMES MDEE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:-

Je, makundi gani yamenufaika na mkopo wa Shilingi Trilion 1 ulioahidiwa kutolewa na Serikali katika Sekta ya Kilimo na kwa masharti gani.

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

**19. MHESHIMIWA HAWA MCHAFU CHAKOMA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, ni Wanafunzi wangapi waliokuwa wajawazito na wangapi wamerejeshwa shuleni baada ya agizo la Mheshimiwa Rais.

**VII. HOJA ZA KAMATI:**

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU:**

Kwamba, Bunge sasa lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2022.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI:**

Kwamba, Bunge sasa lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2022.

**DODOMA**
**31 JANUARI, 2023**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc***
**KATIBU WA BUNGE**